KUHESABU KINYUMENYUME

Sasa, tumechelewa kama dakika thelathini, dakika thelathini na tano hivi. Nitahubiri ila kwa muda mfupi tu, maana tutakuwa na mstari wa maombi, tukiwaita watu wote walio na kadi zao za maombi, na kuwaombea. Hiyo ndiyo ahadi yetu.

2 Lakini sasa tunasimama kwa kuliheshimu Neno, wakati nikisoma sehemu ya Maandiko hapa, na kumwomba Mungu anipe msingi wa somo langu. Tunafungua Waebrania, mlango wa 11, kama ungetaka kufuata tunaposoma.

> *Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*
>
> *Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa.*
>
> *Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.*

3 Na tuombe. Bwana, bariki Neno Lako. Takasa chombo ambacho kitatumiwa nalo. Na jalia chombo kiambatane na Neno, kuleta Uzima na kulifanya Neno hili liishi tena mbele zetu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

4 Sasa nipeni tu usikivu wenu kamili kwa muda mfupi tu, kama dakika ishirini. Nina somo fupi hapa, ningetaka kuliita: *Kuhesabu Kinyumenyume*.

5 Mnajua, pamoja na mambo yote hayo, je! mlisikia kile Maandiko yalichosema? Vitu vilivyopo, tunavyoviona, vilifanywa kwa vitu visivyo dhahiri, kwa maana ilikuwa ni Neno la Mungu Ambaye aliyenena vitu vikawa. Dunia tunayoikalia leo, viti tunavyokalia, sakafu iliyo chini yetu, mavumbi, miti, kila kitu, si kitu ila ni fasiri ya Neno la Mungu. Mungu anapolifasiri, linapotukia, hilo linafunua kitu hicho. "Na iwe," na ikawa. "Na iwe," na ikawa. Na kuona maumbile, jinsi yalivyofanyika.

6 Sasa, maumbile yamekuwa ndiyo Biblia yangu. Kama vile kila mtu anavyojua, ambaye mimi nimeninii. . .wamekuwa katika kusanyiko langu, nilipozungumza, kweli mimi niko karibu upande wa wasiosoma, na ninasoma kwa shida sana. Nilikuwa na elimu ya darasa la saba. Nimepitia mengi maishani mwangu. Lakini, katika kuhubiri kwangu, inanibidi kuchukua uvuvio wangu na kuufananisha na kitu fulani katika. . .katika maumbile, ili kwamba mweze kufahamu yale ninayozungumzia. Siwezi kutumia maneno kama mtu mwerevu, mwenye elimu anavyofanya, kwa maana sina elimu ya kufanya jambo hilo

nayo. Kwa hiyo basi ninachukua maumbile, na kufananisha yale uvuvio wangu unavyoniambia, na maumbile. Nilijisikia mpweke sana, kwamba, lakini wakati mmoja . . . nilisoma katika Biblia ni pale ambapo manabii wa Agano la Kale walipofanya jambo hilo.

7 Na halafu nabii aliyekuwa mkubwa kuliko wote alikuwa ni Yohana. Nasi tunaona, wakati alipokuwa na umri wa miaka tisa, alichukuliwa akapelekwa jangwani na Roho, kwa maana alikuwa amtambulishe Masihi. Baba yake alikuwa ni kuhani. Ilikuwa, kwa kawaida, ya kwamba yeye—yeye angefuata mwelekeo wa baba yake. Lakini, kazi yake ilikuwa muhimu mno, kuchukua maadili ya yale ambayo mtu mwingine aliwazia. Ilimbidi kupata ujumbe wake kutoka kwa Mungu. Kwa hiyo, kwenye umri wa miaka thelathini yeye alitoka jangwani, bila elimu, bali akiwa na ari motomoto moyoni mwake, akiwa na ufunuo kutoka kwa Mungu, na ono, ya kwamba alikuwa amtangaze Masihi. Alijua jambo hilo waziwazi sana, mpaka akasema, "Kuna Mtu anayesimama miongoni mwenu, sasa hivi, ambaye hamumjui." Wazia jambo hilo. "Mtu anayesimama kati yenu, papa hapa, ambaye hamumjui. Yeye, viatu vyake sistahili kuvifungua, bali atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto. Pepeto Lake liko mkononi Mwake."

8 Na je! mliona na—namna yake ya mahubiri? Sasa, yeye aliwaambia Mafarisayo walipojitokeza kwenda. Yeye alijua, akiwa ni nabii, alijua yale yaliyokuwa moyoni mwao. Naye alisema, "Enyi wazao wa nyoka," akimaanisha majoka. Unaona, wao, alijua ya kwamba hilo . . .

9 Sasa, watu wengine huenda wangalisema, "enyi," kitu kingine, unajua, walitumia baadhi ya . . . m—msamiati mzuri, sarufi sanifu, "Enyi kipingiti bure kidogo chenye tafshani," ama chochote kile ungetaka kukiita. Hilo huenda likawa si sahihi; nililichukua tu hilo, unaona. Kwa hiyo huenda yangalikuwa ni maneno mengine ambayo angaweza kutumia.

10 Lakini, unaona, uvuvio wake, yeye alijua ya kwamba nyoka alikuwa ni maskini kiumbe duni, na kibaya, na kijanja. Kwa hiyo alisema, "Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja? Msianze kusema mioyoni mwenu, ya kwamba, 'Sisi ni wafuasi wa *hili*, ama *lile*,' kwa maana nawaambia, ya kwamba Mungu anaweza kutoka katika miamba hii, mawe," yale aliyokuwa ameona jangwani na ufukoni, "kumwinulia Ibrahimu watoto. Pia, shoka limekwisha kuwekwa kwenye shina la mti." Kile alichokuwa ameona. "Kila mti," kama vile ilivyokuwa kule nyikani, "ambao haukuzaa tunda," hiyo ndiyo aliyotumia kwa kuni. Unaona, "Na limewekwa penye shina la mti! Na kama halizai tunda zuri, linakatwa na kutupwa motoni." Unaona, uvuvio wake uliandamana na maumbile.

11 Na—na kama ungeangalia maumbile kwa makini sana, hutaenda mbali sana na Neno, kwa kuwa Mungu yuko katika

maumbile. Nafikiri, mara ya mwisho nilipokuwa huku kwenye Pwani ya Magharibi, nilihubiri juu ya njia nne za kumwona Mungu; Mungu katika Mwanawe, Mungu katika Neno Lake, Mungu katika maumbile, na kadhalika.

12 Sasa kama tukiangalia kila kitu ambacho Mungu alikifanya katika maumbile, kwa kuwa nitazungumza kwa namna hiyo, juu ya vitu vya maumbile ya kawaida vikiwa ni mfano wa vitu vya mambo ya kiroho, hivyo . . . kwa sababu vilifanywa kwa vitu visivyo dhahiri. Ilikuwa ni Neno. Sasa tunachukua kwa mfano kitu kama . . .

13 Miezi michache iliyopita, niliombwa kuhubiri somo, somo la mazishi, kwa ajili ya rafiki wangu mpendwa wa zamani. Wengi wenu mlisoma kitabu changu, na mnakumbuka pale ambapo mimi . . . mvulana mmoja ambaye alininii . . . mmoja aliyekuwa ni baadhi ya maskauti wavulana, ama chochote kile, naye . . . nilimwomba aniwekee ninii yangu . . . aniwekee ninii yake ya zamani ya kao- . . . ama—ama suti ya skauti, atakapoichakaza kwa kuivaa. Vema, aliniwekea soksi ndefu ya mguu mmoja. Mnakumbuka jambo hilo, kwenye kile kitabu. Nami nikaivaa. Lloyd Ford, mama yake alikufa hivi karibuni, akiwa na umri wa karibu miaka themanini na mitano, rafiki yangu wa thamani sana. Na Lloyd, akiwa bado hajaoa, naye alikaa na mama yake, alinijia. Naye akasema, "Ndugu Bill." Hivyo ndivyo alivyonijua. Sisi, nilimwita Lloyd, aliniita Bill.

Basi nikasema, "Unataka nini, Ndugu Lloyd?"

Akasema, "Je! utaninii—utahubiri kwenye mazishi ya mama?"

14 Nikasema, "Ningefurahia kufanya hivyo. Ingekuwa ni kama mama yangu mwenyewe, hata hivyo." Nikasema, "Amenipikia milo mingi sana, na kadhalika, na amekuwa na upendo sana kwangu."

15 Akasema, "Ninakutaka wewe useme yale maneno ya mwisho kuhusiana naye, Ndugu Branham."

16 Nikasema, "Ungeninii—ungetaka niseme nini, Lloyd?"

17 Alisema, "Jambo moja ninalotaka ufanye. Wahakikishie tu watu wangu, tuhakikishie juu ya kufufuka kwake."

18 Kwa hiyo nikachukua somo kutoka mahali fulani katika Ayubu, jinsi ambavyo Ayubu alikuwa akiangalia maumbile. Nami nikasema, katika ninii yangu . . .

19 Kifo cha mama yangu mwenyewe, mama yangu mwenyewe ambaye alikufa karibuni kama miaka miwili iliyopita. Dada yangu mdogo alikuwa tu ndiyo kwanza aokoke, muda si mrefu, naye alinipigia simu wakati alipojua mama alikuwa anaaga dunia. Naye akasema, "Bill, nifanyeje?" Kasema, "Siwezi kamwe kuvumilia jambo hilo tena, kusimama pale nikimwangalia mama yangu."

Nikasema, "Ndilo tamasha la kupendeza sana nililopata kuona."

Akasema, "Unawezaje kusema jambo hilo, na, ni mama yako?"

20 "Loo," nikasema, "yuko tayari kuondoka, na anataka kuondoka. Yeye ni mzee, naye yuko tayari kutoka katika maisha haya."

21 Nikamwambia, "Mama, je! Yesu angali anamaanisha kwako . . . Alivyofanya siku uliyompata Roho Mtakatifu?"

Angesema, "Ndiyo." Wakati, nami ningeninii . . .

Wakati asingeweza kufanya hivyo tena, nilisema, "Hebu tabasamu."

22 Wakati alipokuwa amedhoofu sana, asingeweza kutabasamu wala kuzungumza, nilisema, "Mama, unakufa." Alikuwa mikononi mwangu. Nikasema, "Mama, kama Yesu Kristo angali anamaanisha vile vile kwako, na yungali ni mtamu vile vile, ama hata ni mtamu kuliko alivyokuwa wakati ulipompokea Roho Mtakatifu. Mimi ni mwanao mhubiri. Sina budi kukutana na watu. Je! Yesu anamaanisha jambo fulani kwako, wakati unakufa? Kama ndivyo, kama huwezi kuzungumza . . . " Wala asingeweza kuzungumza. Nikasema, "Je! huwezi kuzungumza, mama?" Asingeweza kusogea. Nikasema, "Pepesa macho yako, upesi sana." Ndipo akaanza kupepesa macho yake upesi sana, na maji yakitiririka chini ya mashavu yake. Wakati asingeweza hata kuzungumza tena, lakini hisi zake ndani yake zilihisi Uwepo wa Yesu Kristo. Mnamo dakika chache, Upepo ulikuja ukapita kote chumbani, na mama akatoka pamoja nao, kukutana na Mungu.

23 Sasa, mwanamke huyu wakati alipokufa, nilisema, "Je! kuna matumaini katika ufufuo?" Nikasema, "Kila kitu . . . "

24 Nimejaliwa kuhubiri karibu kwa kila taifa chini ya mbingu. Nimeona miungu ya kila namna na dini za kila namna, bali hakuna hata moja ya hizo iliyo ya kweli ila Ukristo. Ndiyo pekee yake. Hata maumbile, yenyewe, yanazungumza juu ya Ukristo, Mungu Muumba!

25 Angalia, kuna uzima, mauti, mazishi, ufufuo. Ufufuo! Ninii yote . . . Huwezi kutoka huko nje bila ya kuona jambo hilo. Angalia majani yakichipuka katika msimu wa kuchipuka. Yaangalie yakifikia ujana wao katika uzee wao, katika umri wao wa makamu, na halafu umri wao wa uzeeni. Na vile vishipajani katika majani, vikibeba uhai. Dakika chache, unaona si muda mrefu, kabla theluji nyembamba yoyote haijaanguka ama chochote kile, hayo majani yanapukutika. Na nini kinachotendeka? Uhai ule ulioko kwenye mti huo, utomvu huo, hushuka ukaingia kwenye mizizi. Kama haukuingia, baridi ya kipupwe ingeuua mti huo, itaua uhai huo. Hauwezi kukaa juu.

Hauna budi kushuka chini na kujizika. Lakini katika msimu wa mwaka wa kuchipuka majani, huu hapa unarudi, ukiwa na tawi jipya tena. Unashuhudia kuna uhai, mauti, mazishi, ufufuo. Kila kitu kinafananisha. Hatuwezi kabisa kuachana nalo.

26 Angalia jua linapochomoza asubuhi, jua lile linaloangaza mbingu. Ni mtoto mchanga, anayepembezwa mikononi mwa mama yake, wakati ni mdhaifu, hana uhai mwingi, hana nguvu sana. Na halafu yapata saa mbili, linaanza kwenda shuleni. Saa tano na nusu, limehitimu, na limetoka shule ya sekondari ya juu na kutoka chuoni. Ndipo limefikia kilele cha nguvu zake, kutoka karibu saa sita mpaka karibu saa nane. Ndipo linaanza kudhoofika, linadhoofika zaidi, zaidi, zaidi, na hatimaye linakuwa dhaifu kwelikweli kama mzee ama ajuza, linatua. Je! huo ndio mwisho wake? Linarudi kesho yake asubuhi kushuhudia, "Kuna ufufuo, na uhai ng'ambo ya pili ya mauti."

27 Kila kitu kikishuhudia. Maumbile yote yanashuhudia. Neno linashuhudia jambo hilo. Roho Mwenyewe aliye moyoni mwetu, anashuhudia jambo hilo. Kitu fulani ndani yetu, kinaita, kwamba, "Kuna ufufuo wa wafu." Kwa hiyo, unaona, kusema . . .

28 Kama kila kitu kinatumikia kusudi la Mungu, kina ufufuo. Bali kinaweza tu kufufuka kama kinatimiza kusudi la Mungu. Kama ua likiishi na halijarutubishwa, halitafufuka tena. Kama ukipanda mahindi, na hayajarutubishwa, hayatachipuka tena. Chochote kisichotumikia kusudi la Mungu, hakina ufufuo. Lakini huwezi kushikilia kitu chochote mavumbini kinachotumkia kusudi la Mungu. Kitafufuka tena na kushuhudia ufufuo. Tunajua ya kwamba mambo haya yote ni kweli. Ni shuhuda kwetu, kututia moyo. Kila siku, kila mahali unakoangalia, unamwona Mungu.

29 Kuna mwili wa maumbile ya kawaida, watu. Kuna Mwili wa kiroho wa watu.

30 Kuna bibi-arusi wa kawaida. Nimekuwa na majaliwa ya kuwaoza vijana na wasichana wazuri. Wala mimi kamwe siwazii jambo hilo isipokuwa . . . Kwa namna fulani mimi huwageuza nyuma, imani ndogo ya aina yangu, nami ninaelekeza nikiwa ninii wangu—mgongo wangu umeelekezwa Mashariki, nao wakiangalia Mashariki. Nami ninapowaangalia, ninawazia juu ya mioyo yao ikipigapiga kana kwamba wao ni mmoja, Kristo na Bibi-arusi Wake. Kuna bibi-arusi wa kawaida, na kwa kuwa kuna bibi-arusi wa kawaida, ni ushuhuda tu kuna Bibi-arusi wa kiroho. Kuna Bibi-arusi wa kiroho, kwa maana kuna bibi-arusi wa kawaida.

31 Matukio haya yote ya kawaida, sasa, yanatangulia mambo ya kiroho yanayotukia. Kila tukio linaambatana na tukio hilo lingine, ila tu linaliboresha.

Unasema, "Ni kitu gani kinachofanana na hicho?"

32 Vema, kitu kama Uhai wa kiroho, wakati unapoingia kwenye uhai wa kawaida, unauboresha uhai wa kawaida. Hayo, hayo yanakuweka katika hali bora zaidi kuliko uliokuwa nayo katika maisha ya kawaida.

33 Wakati jani linapokauka na linakufa, wakati linaporudi likiwa hai tena katika ufufuo, kushuhudia katika mwaka mwingine, linarudi katika hali bora zaidi kuliko lilivyokuwa nayo wakati liliposhuka chini. Unaona, kila kitu hushuhudia juu ya mambo haya.

34 Sasa hebu na tuchukue, kwa mfano, mafanikio ambayo mwanadamu ameweza kufanya duniani. Katika mafanikio haya yote mambo ya kawaida sasa. . . Ninataka usikivu wenu mkamilifu sasa. Ninii. . . Mafanikio yote ya kawaida yaliyotendeka duniani, yamekuwa ni dalili ya mafanikio ya kiroho ambayo Mungu amefanya kwa njia ya kanisa Lake.

Mambo yote ya maumbile ya kawaida ni mfano wa mambo ya kiroho.

Sasa wewe unasema, "Vipi jambo hilo?"

35 Hebu na tuchukue, mojawapo, usafiri. Kwanza, usafiri ulikuwa ni kwa njia ya farasi. Uliofuata, ulikuwa ni wa motokaa. Ndipo sayansi ikatuundia ndege. Na, lakini, unaona, ni niniii . . . Kwanza, ilikuwa ni nguvu farasi moja. Gari lilikuwa labda ni nguvu-farasi ishirini. Ndege inafikia mamia ya nguvu-farasi. Mnaona ni kitu gani? Ni kama tu vile tumekuja na farasi, halafu motokaa ikaundwa, ndipo kitu kilichofuata kilikuwa ni ndege. Tunaendelea tu kufanikiwa, juu zaidi na zaidi, vikizidi kuwa vikuu zaidi na zaidi. Haya ni mafanikio ya sayansi. Hii ni dalili ya mambo ya kiroho yaliyotukia, ya Mungu, kwa Roho Wake, yamekuwa katika Neno Lake lililoahidiwa.

36 Mtu wa maumbile ya kawaida, kwa maarifa, huangalia nyuma kwa mafanikio yake; hiyo ni sayansi, kuona yale Mungu amefanya katika maumbile ya hapo nyuma. Wanatoka kwenda kuokota madonge ya udongo, na kuokota vipande vya miamba na visukuku, na—na elementi mbalimbali, na kuunganisha vitu hivyo pamoja. Unaona, katika kufanikiwa huko, wanachukua kile Mungu alichokwisha umba, na kukipotosha kutoka katika hali yake ya asili, na kuyafanya makazi yake ya kuishi, na kadhalika, na uchumi wake mzuri kidogo zaidi, kwa yale ambayo yamekwisha kuumbwa. Hayo ni katika mafanikio ya kawaida, ya mwanadamu.

37 Bali Mungu, katika mafanikio ya kiroho, anasonga mbele, si kurudi nyuma. Yeye mwanadamu anasonga mbele, akiangalia katika Neno, na kuamini ahadi kwa mambo ambayo hayajakuja bado, kwa ufunuo wa kiroho ili kudhihirisha mambo ya kiroho ambayo Mungu ameahidi. Anayaona yakitimia. Kama tu vile mwanasayansi katika maabara yake wanavyofanya kazi kwa mambo mbalimbali kumsaidia mwanadamu, wakichukua

maumbile; mtu wa kiroho anatazamia kitu ambacho Mungu aliahidi, ambacho hakijaumbwa bado. Mtu wa maumbile ya kawaida huangalia nyuma. Mtu wa kiroho huangalia mbele.

38 Hivyo ndivyo ilivyo, wana—wana jambo hilo kanisani. Mtu wa kawaida wa kanisa anaangalia nyuma kwa yale Finney, Sankey, Knox, Calvin. Hayo yalikuwa ni sawa, bali hayo yalikuwa ni kwa ajili ya siku yao. Tunatazamia kitu kingine, ahadi ambayo ni kuu zaidi na ya juu zaidi, na yale Mungu aliyoahidi. Sayansi hurudi nyuma, kulichukua. Sisi tunasonga mbele, katika Neno la Bwana, kuona ni ktu gani Mungu amefanikisha.

39 Katika mambo haya mawili, moja linatangulia lingine, ama huonyesha mfano wake. Sasa kama vile sayansi ilivyoweza kufanikisha kuongeza nguvu-farasi zaidi, kama binadamu alivyofanya kwa kuchukua zile nguvu na kutengeneza vyombo vikuu zaidi, motokaa na ndege; Mungu amefanikisha kwa njia ii hii, kama vile kila moja ya mifano hiyo ilivyo. Sasa angalia.

40 Huko nyuma kabisa katika siku za Luther, nguvu zao zilikuwa ni nguvu-farasi. Na halafu Mungu, kwa kumchukua Luther mikononi Mwake, alimwongoza, kutoka katika shirika kubwa, ama mfumo, Yeye alimruhusu mtu huyo kuona ya kwamba "mwenye haki ataishi kwa imani." Na wakati alipoweza kufanikiwa katika jambo la kuhesabiwa haki, na kukuhubiri, kanisa likafufuka likawa Hai. Lilifufuka na likaanza kusonga mbele kidogo tu, huko zamani katika siku za nguvu farasi, wakati nguvu farasi zilipokuwa ziko karibu na kutoweka, za gari la farasi, na farasi na kigari chake. Sasa, yeye alifikia kuhesabiwa haki, na, kwa huko, ndipo kanisa likapokea Uhai kwa kumwamini Yesu Kristo. Si kuchukua baadhi ya ninii . . .

Unasema, "Ninaamini kanisa. Ninaamini jambo *hili*."

41 "Kumwamini Yeye ndio Uzima." Kuhesabiwa haki kwa imani! Luther alikuhubiri. Huko kulifananishwa na siku za usafiri wa farasi na kigari chake.

42 Ndipo akampata mtu mmoja huko Uingereza, jina lake John Wesley, chini ya mamlaka yake, kuondoa itikadi hizi zote, toka kwake. Naye aliweza, kwa kumtumia John Wesley, kuingiza utakaso kanisani. Utakaso ulilisimamisha kanisa kwa miguu yake na kulifanya liweze kutembea. Sasa mwishoni mwa wakati wa Wesley kulikuwa na motokaa, tunatambua ya kwamba wakati ninii . . . mwishoni mwa kanisa la Wesley, ninamaanisha. Si . . . Unaona, kila—kila mtengenezaji huja mwishoni mwa wakati. Sasa tunaona ya kwamba Wesley, katika sehemu ya mwisho ya wakati wake wa kanisa, uliingia tu kabla ya Wapentekoste. Mbona, tunaona ya kwamba kanisa lilipata nguvu za kutosha, kupitia utakaso, kuyaacha mambo ya ulimwengu. *Kutakasa* maana yake ni "kutenga kwa ajili ya

utukufu wa Mungu." Ni vibaya sana kwamba lilipoteza hilo. Bali lilipata nguvu za kutosha.

Luther alilipa nuru, huko nyuma katika siku za usafiri wa farasi na kigari chake.

43 Wesley alililisimamisha kwa miguu yake, likaanza kutembea; utakaso, likijitenga na mambo ya ulimwengu. Kutokana na hilo kukatokea matawi madogo, kama vile Pilgrim Holiness, na Wanazarayo, na wowote wale wengine kutokana na hilo, kwa utakaso.

44 Lakini, kumbukeni, wasingeweza kutulia. Nguzo ya Moto iliondoka. Nao wakafikia kwenye Mtaa wa Azusa, hapa California. Na basi ilifanya nini? Iliwakilisha siku za ndege, kutoka kwenye motokaa, wakati wao . . . Mungu aliweza, kwa wale Ndugu wa Wright, kuninii . . . ama mwanadamu aliweza, kufaulu kutengeneza ndege ambayo ingeweza kuruka. Mara, kutangulia hayo, pentekoste ya Mtaa wa Azusa ilishuka, na mwanadamu akaruka kwenda hewani, akaingia katika mambo ya mbinguni, kwenye yasiyojulikana. Alinena kwa lugha zisizojulikana, akafanya mambo yasiyojulikana yaliyokuwa ni mageni kwa kanisa, kwa maana alikuwa ameruka akatoka ardhini, alikuwa ameruka (hewani) akaingia hewani. Ilifanya nini? Mara baada ya hizo ndege kuja, yeye aliruka akaenda hewani. Mungu alionyesha, kwa hizo ndege, ya kwamba kanisa Lake lilikuwa likiinuka. Anaonyesha, kwa mambo ya kawaida, yale yanayotukia katika ya kiroho. Daima hufuatana. Ni kama tu vile wale mamajusi wakiifuata ile Nyota, wakimtafuta Kristo, baada ya kuifuata kwa muda wa miaka miwili.

45 Sasa angalia, mambo hayo yote ni mafanikio ambayo mwanadamu amefanikisha, ni kwamba tu hiyo ni mifano na vivuli vya yale Mungu anayofanya. Yeye hufanya hivyo daima. Ametwambia ishara ambazo zingetokea mbinguni, mambo ambayo yatakuwa yakitukia kabla tu ya kuja kwa Kristo. Tunaona jambo hilo sasa. Ni nguzo tu ya kuelekeza. Nasi tunaona sayansi, jinsi ambavyo wamefanikiwa, na jinsi ambavyo Mungu amefanikiwa kwa kanisa Lake.

46 Je! mtu anapanda ndege? Hataki usafiri wa farasi na kigari chake tena, isipokuwa awe anataka tu kujifurahisha kidogo. Lakini farasi na kigari chake . . . Kumbukeni, nguvu zilizoko ndani ya ndege ni nini? Ni farasi zaidi tu walioongezwa, ni hivyo tu.

47 Na kwa hiyo wakati John Wesley alipopata utakaso, kazi iliyotengwa mbali na kuhesabiwa haki, yeye kamwe hakutupa kuhesabiwa haki, yeye alikuongezea tu nguvu zaidi. Mnaona?

48 Na wakati Wapentekoste walipopata ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kurudishwa kwa karama, hawakukana utakaso wala kuhesabiwa haki, walipata tu nguvu zaidi na wakainuka, na wakapaa juu kwa sababu mtu kapata nguvu zaidi. Mnaona?

49 Mambo hayo yote yakionyesha kivuli, jinsi yalivyokuja. Kama tungalikuwa na wakati, kweli tungelidumu katika jambo hilo, bali hatuna. Lakini mtu alipaa juu. Kama vile sayansi ilivyofanikiwa na jambo fulani, ikiangalia nyuma; Mungu hufanikiwa, akienda *huku*, akienda mbele kwenye ule Ufalme.

50 Sasa tunaona, kutoka katika Mtaa wa Azusa, ndege ziliruka katika ule ufufuo mkuu, na kusambaa ulimwenguni, kwenye yasiyojulikana, zikaingia katika ulimwengu wa Roho, wakinena kwa lugha zisizojulikana, wakiwa na karama zisizojulikana, kwa ulimwengu. Mbona, wao walifikiri walikuwa ni walokole, bali walikuwa wameweza. . .Mungu alilishika kundi la watu mikononi Mwake. Kisha akamchukua maskini Mnegro mwenye makengeza, hapa chini kwenye Mtaa wa Azusa, ambaye hakuwa na wazo lingine ila kuamini yale Mungu aliyosema ni Kweli. Na hiyo ni kweli.

51 Unaona, wakati inapoibidi sayansi kuweka mawazo mengi katika kichwa cha mwanadamu, ya hekima, ya maarifa, kurudi nyuma na kupata mambo haya; Mungu hana budi kuchukua yale aliyo nayo, ayatoe kwake, kusudi aweze kumtumia. Mmoja anaenda *hivi*, na huyo mwingine anaenda *vile*. Mmoja anashuka, na huyo mwingine anapaa juu.

52 Sasa, yeye aliacha haya makanisa ya kielimu yamekwama, wakati Pentekoste ilipoondoka ikiwa na kunena kwa lugha na karama kuu za uponyaji. Waliwaponya wagonjwa. Walifanya mambo makuu. Wameyafanya. Hapana shaka ila kwamba wameyafanya. Ni thibitisho, ya kwamba wameyafanya. Hakika waliyafanya! Nao wakaliacha kanisa hili la kielimu limeketi kitako ardhini. Haidhuru, wanasema, "Vema, huwezi." Walifanya jambo hilo, hata hivyo. Kama ninyi mnaninii . . .

53 Ni kama yule mvulana mdogo huko gerezani, kwa ajili ya kupiga mbamia risasi. Mtu fulani aliingia, akasema, mvulana mdogo alikuja kumtembelea, kasema, "Loo, hawawezi kukufunga gerezani kwa jambo hilo!" Akasema, "Ati hawawezi?" Alikuwa yuko huko tayari.

54 Na hivyo ndivyo wanavyosema, ya kwamba, "Roho Mtakatifu alikuwa ni kwa wakati wa huko nyuma." Hivyo ndivyo wanavyofikiri! Yupo hapa! Tunajua jambo hilo. Sisi, na—na ni ninii. . .Tumekuwa tukiruka hewani kwa miaka arobaini, hamsini iliyopita, Naye, tukiona mambo ambayo wasomi hawajui lo lote kuyahusu. Jambo tu wanaloweza kufanya ni kuketi chini na kusema, kulidhihaki tu.

55 Kama vile ndama mdogo, wakati mmoja, alipotoka kwenye zizi, wao walisema, na alikuwa tu mnono na mnene. Alikuwa akirusha mateke yake. Naye alikuwa na mfugaji mzuri sana aliyemlisha vizuri, naye alikuwa mnene sana na amejaa vitamini. Na mkulima mwingine mzee goigoi kule aliyekuwa na ndama mdogo, pia, aliyezaliwa kwenye banda wakati huo wa kipupwe,

wakati maskini jamaa huyo mdogo hakuwa amekula kitu ila majani. Na wakati alipotoka, alikuwa amekonda sana ilikuwa ni vigumu kwake kutembea, na, kila wakati, upepo ungevuma na kumsukuma kando. Aliona ndama huyu mdogo wa mtindo wa kale akitupa tu mateke, na akiwa na wakati wa furaha sana. Mwajua, aliangalia tu kupitia kwenye ufa wa ua, na kusema, "Ulokole wa ji—ji—jinsi gani huo!" Alikuwa amejaa vitamini, si ajabu angaliweza kutupa mateke yake.

56 Na wakati mtu amejazwa na Roho Mtakatifu, kuna kitu fulani ndani yake, ambacho kimejaa Vitamini ya kiroho ya Mungu, inayomfanya amsifu Mungu, apige makelele, na kutenda isivyo kawaida. Kwa kuwa nini? Yeye si wa duniani tena. Yeye yuko Mbinguni, akisafiri kwenda zake huko, katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu.

57 Aliwaacha wakiwa wamelemewa duniani pamoja na baisikeli zao na motokaa zao, wameingia hewani. Naam, bwana. Kwa kweli amewatoa kule kabisa, wamepitwa na wakati. Waliwaponya wagonjwa. Walinena kwa lugha zisizojulikana, na kufanya mambo mengi.

58 Lakini sasa, enyi marafiki, hebu niseme jambo hili. Imefikia wakati wa wanaanga. Tumetoka kwenye wakati wa ndege. Tuna nguvu zaidi sasa. Wakati wa wanaanga umeingia. Ni kitu gani? Si ninii . . . Tumeingia katika wakati wa kiroho wa mwanaanga, unaona, tukienda juu. Si ninii . . . Ni roho yeye yule, ila tu ana nguvu nyingi zaidi, ametuinua juu zaidi, tunaweza kupaa juu zaidi, kuona mengi zaidi, kuamini mengi zaidi, kufanana zaidi sana na Kristo. Si motokaa, si farasi na kigari chake, si hata ndege, bali, mwanaanga, yeye anaruka juu na kupita kila mmoja.

59 Unaitwa wakati wa tai, katika Biblia. Mungu anawaita manabii wake . . . Wakati wa tai! Tunatambua, humu katika Biblia, tunaona, katika Malaki 4, ya kwamba tuliahidiwa hilo katika siku za mwisho. Sasa, Yeye anawalinganisha manabii Wake na tai. Anajiita Yeye Mwenyewe tai. Yeye ni Yehova tai mkuu.

60 Yeye anaweza kujiletea, Kwake Mwenyewe, Bibi-arusi. Atafanya hivyo, katika siku za mwisho, ataweza kupata Bibi-arusi, aliye na huduma ambayo inafanana kabisa, ninii . . . kama vile mtu na mkewe huwa mmoja. Na wakati Yehova atakapowafanya watu Wake kuwa kama Yeye, ndipo Yeye anaishi katika watu Wake. Wote ni mmoja.

61 Inatimiza Maandiko, sawasawa kabisa na vile Yeye alivyosema katika Yohana Mtakatifu 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Pia inatimiza yale Yesu aliyosema yangetukia, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu."

62 Sasa ni wakati wa mwanaanga. Na mwanaanga huona vitu ambavyo mpanda farasi, motokaa, ama ndege, wote hao, huona. Yeye huruka juu zaidi. Ndege ingali ipo hapa chini ikirukaruka mawinguni, na ikizimikazimika, na kuanguka chini, na chochote kile. Bali yeye anapaa juu kupita mawingu ya kanuni za imani na madhehebu, anaenda juu zaidi anaingia Mbinguni, moja kwa moja mbali na kila kitu.

63 Wakati wa mwanaanga, tunaishi katika wakati wa mwanaanga. Kwa hakika tu kama vile Mungu ameshuhudia kwa matukio ya kawaida pale, vivyo hivyo Yeye anashuhudia sasa ya kwamba, kama tumefikia kwa mwanaanga, Mungu amefanikishwa na yale aliyoahidi kufanikisha katika siku za mwisho, kulingana na Malaki 4. Jambo pekee linalombidi kufanya ni kumpata mtu mikononi Mwake, ambaye anaweza kujiondoa kwenye ndege na motokaa, na chochote kile. Si kuangalia nyuma kwenye yale yaliyokuwako, bali nguvu zaidi za kumwinua juu zaidi, kumwinua zimwingize katika Uwepo wa Mungu, kumwinua kule juu ambako mambo yote yanawezekana. Sasa tunaona jambo hilo likitukia. Hakuna shaka kwake.

64 Ndivyo alivyo mwanaanga wa kiroho, kama vile mwanaanga wa kawaida anavyopaa juu ya ndege; ndege daima zikipata ajali, zikipigana huko mawinguni, na kila kitu namna hiyo. Hakuwezi kuwa na kitu kingine kilicho kikuu zaidi, hakuna maendeleo ya zaidi, kuliko ya mwanaanga. Jambo tu yeye analopaswa kufanya ni kuendelea tu kuongezea nguvu nyingi zaidi, ataenda popote atakapo, unaona, kwa kuwa tayari ameingia katika anga. Ndege zingali ziko chini, zikipata ajali, zikizozana, zimeharibika, na kila kitu namna hiyo. Bali mwanaanga haimbidi kuharibikiwa. Anapaa juu zaidi ya mawingu. Anapaa juu, juu ya kanuni za imani, juu ya madhdhebu, juu ya hao wasemao, "Sivyo ilivyo, sivyo ilivyo!" Yeye ana kiongozi, Roho Mtakatifu. Neno linamwambia hivyo, naye anasonga mbele!

65 Sayansi inambunije mwanaanga? Yeye huchukua nguvu walizo nazo, na kuendelea tu kuvunjavunja kitu fulani ndani yake, kitakifanya kiende mbali zaidi, kiende bila hewa, na kadhalika. Anaendelea . . . Sijui ke—kemikali zake; mimi si makanika. Lakini chochote kile, yeye huendelea kukifanya kipae juu zaidi na zaidi. Yeye huendelea kukiboresha wakati wote, mpaka sasa anaweza kwenda kupita hoja yoyote. Vivyo hivyo na mwanaanga wa Mungu, huenda kupita mbele ya kanuni zote za kanisa, mipaka yote, mambo yote haya yanayosema, "Siku za miujiza zimepita; hakuna kitu kama hicho."

66 Mwanaanga alilipataje jambo hili? Alilichora kwenye karatasi. Likatoka kwenye karatasi, lile alilokuwa amewazia. Ni jambo lile lile, kwamba mtu yeyote anaweza kuketi chini na kusoma Neno la Mungu na kuona yale yaliyoahidiwa. "Yachunguzeni Maandiko, ndani Yake mnafikiri mna Uzima wa Milele," Yesu alisema, "nayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi."

Kundi hilo lililotekwa na dunia walilokuwa nalo kule nyuma katika siku hizo halikujua kwamba Yeye alikuwa ni nani.

67 Huduma, kile kinachoifanya, mwanaanga huona vitu, ambapo ndege na kila kitu vimepitwa na wakati. Vivyo hivyo na mwanaanga wa kiroho, anaenda kupita mawingu na kupita kanuni za imani, na kupita mashaka, anaingia kwenye anga la nje; anga za juu, la kutokuamini kote, anga za juu ambako hasikii piga domo lisemalo, "Vema, huwezi kufanikiwa. Hakuna mtu atakayeshirikiana nawe, atakayeshirikiana nawe. Huwezi kufanya *hivi*. Huwezi kufanya *vile*." Yeye haoni hilo. Yeye ni mwanaanga. Anaenda kupita yale mawingu. "Kuna hali mbaya sana ya tufani. Hatuwezi kusafiri." Haileti tofauti yoyote kwa mwanaanga; yeye huenda kupita ile tufani. Unaona, hivyo ndivyo ilivyo kwa imani ya mwanaanga halisi leo. Wao wanasema, "Vema, daktari alisema *hivi na vile*." Hilo huenda likawa ni sawa, bali mwanaanga haamini jambo hilo.

68 Wakati limeandikwa Hapa, yeye analo Hilo moyoni mwake. Kitu fulani kinamwambia, yeye anakiendesha moja kwa moja huku kwenye anga. Hivyo tu. Anaenda moja kwa moja kuingia angani, kwa maana tunaishi katika wakati wa mwanaanga, naam, bwana, huko nje angani, "ambako mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio." Yeye ana kiongozi, ambaye ni Neno Lake, ambalo linamwambia jinsi ya kwenda, Neno la Mungu.

69 Mwanaanga wa kawaida ni . . . ana kitu fulani cha kumwongoza. Wakati mwanaanga akiwa yuko hewani, ana kitu fulani hapa nyuma, huku nyuma duniani, kinachomwongoza. Kinaitwa rada. Rada hiyo inamwongoza kote, inamwonyesha mahali alipo, inamwambia yale anayofanya. Na rada hiyo inamwongoza kutoka kwenye mnara wa rada, hapa duniani. Huyo ni mwanaanga wa kawaida.

70 Vivyo hivyo na mwanaanga wa kiroho ana Nguvu zinazomwongoza, ana mnara wa kumwongoza, pia. Hauko hapa *chini*, kama wa mwanadamu ulivyo. Uko huko Juu. Nao ni Roho Mtakatifu aliye ndani yake, ambaye anamwongoza, mnara wa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unamwongoza, unamwongoza kwa Neno; si katika tita la ushupavu wa dini, upuuzi fulani uliochochewa, bali, BWANA ASEMA HIVI, na linatukia. Daima unamthibiti. Yeye ana mnara wa kuongoza, huyo ni roho Mtakatifu. Na Neno ndilo mpango Wa—Wake, naye hushikilia kwenye mpango huo moja kwa moja. Na nguvu za Roho Mtakatifu zinampa uwezo wa kuendelea, na uwezo huo unaleta mafanikio ambayo Mungu anataka yafanikishwe kwa ajili ya watu Wake, lipate kutimiza kile Yeye alichoahidi.

71 Yesu hakuwaponya watu kwa sababu ilimbidi kufanya hivyo. Alitimiza jambo, alitimiza Maandiko. Aliponya kwa sababu iliandikwa angefanya hivyo. Haimbidi kuonyesha ishara hizi leo.

Haimbidi kuwa na huduma *fulani*, bali Yeye aliahidi angefanya hivyo. Anafanya hivyo kutimiza ahadi Yake.

72 Ndugu, dada, mwanamume, wanawake, hivi hamwezi kuona jambo hilo? Hamwezi kuona mfano wa ya kiroho, na wa ya kawaida?

73 Mafanikio haya makuu yameleta wakati wa saa ya sayansi, na ilivunja na kuingia mahali fulani mpaka wao wanasema sasa ni ninii tu. . . Kwenye saa ya sayansi, wanasema ni usiku wa manane kasoro dakika tatu. Wako wakati wa mwisho. Wamegundua kile kitu ambacho kitawaangamiza. Wamegundua kila kitu. Mwanaanga anaweza kuingia hewani na kwenda sehemu fulani, kwa nguvu za atomiki, na kukaa huko na kusema, "Jisalimisheni la sivyo mtalipuliwa." Usiku wa manane kasoro dakika tatu! Wamefanya kazi juu ya yale Mungu aliyoumba. Wameweza kupotosha. Badala ya kujaribu kupata uzima, daima wanajaribu kupata kitu fulani cha kumwua mtu fulani, kitu fulani ambacho kitashinda kitu hicho kingine, kulishinda taifa lingine, kushinda jiji lingine. Hivyo ndivyo wanavyojaribu kufanya.

74 Bali binadamu anaangalia juu, akimwita binadamu ni ndugu yake, na akijaribu kumwongonza kwenye Makao ambako haitambidi kufa. Moja ya makao haya yako katika mauti, hayo mengine yako katika Uzima. Lakini haya, yaliyoko kwenye mauti, yanawakilisha tu Uzima. Jani, linapoanguka kutoka mtini na linakufa, linamaanisha tu litafufuka tena, maana limekwisha kuwako.

75 Saa inagonga, kwenye mafanikio ya sayansi leo, kufikia usiku wa manane kasoro dakika tatu. Kwenye saa kuu ya Mungu, inagonga, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Tumewasili! "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Wakati saa ya sayansi inaposema dakika tatu kufikia maangamizi; saa ya Mungu inasema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Yeye yuko duniani, katika nguvu za Roho Mtakatifu, kulifanya Neno Lake liishi na lifanye kwa ajili ya kanisa Lake yale hasa Yeye aliyoahidi lingefanya, akiwajaza wanaanga Wake, akiwatia mafuta na kuwaweka tayari.

76 Kwa hiyo waliingia katika tyubu yao kuu ya sayansi, hapa si muda mrefu uliopita, tyubu ya mwanaanga, nao wanahesabu kinyumenyume sasa, wakielekea mwezini. Wanaondoka hapa, nao pia. Wana mwanaanga katika tyubu kubwa, inayoendeshwa na nguvu za atomiki, ambayo wanaweza kuituma moja kwa moja mpaka kwenye mwezi, ndivyo wanavyodai. Wamekwishaingia katika tyubu yao na wanangojea kuhesabu kinyumenyume.

77 Mwanaanga wa kiroho aliingia katika Kristo naye anasikiliza kuhesabiwa kinyumenyume kwa Neno. Amina. Sasa ninyi Walutheri mnapaswa kupaaza sauti, na ninyi Wabaptisti

na Wapresbiteri. Angalieni kuhesabu kinyumenyume, kwa Neno. Loo, jamani! Kuhesabu kinyumenyume, kwa Neno! Nao wanaelekea Mbinguni, si mwezini. Watapita mwezi haraka sana hata hawatauona. Loo, jamani! Wanangojea kule kuhesabu kinyumenyume! Naam, bwana. Kungojea kuhesabu kinyumenyume ni sawa.

78 Wao wanafanya nini? Wamefungwa ndani ya Kristo, katika neema ya kunyakuliwa. Hakuna kitu walichofanya, wao wenyewe. Kristo alichukua vitu visivyo na elimu, vijinga vya ulimwengu, akawafunga wanaanga Wake katika hivyo, na kuwapa nguvu za Roho Mtakatifu, wapate kuondoka. Ulimwengu huu utaachwa peke yake. Hiyo ni kweli, kuondoka!

79 Angalieni, mtu wa kawaida hata naye huhesabu kinyumenyume. Nilisema alifanya mambo kinyumenyume. Anahesabu kinyumenyume. Angalia kuhesabu kwake, "Kumi, tisa, nane, saba, sita, tano, nne, tatu, mbili, moja, sifuri!" Unaona, anarudi nyuma, na kuanza kuhesabu. Unaona? Yeye ni ninii sana . . . Kumi ni namba mbaya. Hiyo ni kweli. Kuanzia na kumi, ni namba mbaya.

80 Walikuwa na makabila kumi ya Israeli, na hao wote walikuwa ni wa kimwili tu. Ndipo ilimbidi kuwachukua wana wawili wa Yusufu, Efraimu na Manase, watoto wa nabii, na kuwabariki. Na, wakati alipofanya hivyo, mikono yake ikapitana. Naye akasema, "Baba, sivyo, umeweka mikono yako juu ya Efraimu, inapaswa kuwa juu ya Manase."

81 Akasema, "Mungu alipitanisha mikono yangu." Kutoka ninii . . . Kuzichukua kutoka kwa mwana mkubwa, ile torati, na kuiweka juu ya Kristo. Na kupitia hapo, wakaja, kupitia msalaba likaja badiliko la haki ya mzaliwa wa kwanza, amina, likaingia kwa mwana mdogo. Loo, jamani! Ni ajabu jinsi gani! Kama tungelikuwa na wakati wa kuingilia jambo hilo; tutaliingilia wakati mwingine. Vema.

82 Sasa, kumi ni namba mbaya. Lakini mwanadamu daima huhesabu kinyumenyume, akianzia na kumi. "Kumi, tisa, nane, saba, sita, tano, nne, tatu, mbili, moja, sifuri."

83 Mungu hufanya nini? Anaanza na namba Yake, saba. Hiyo ni namba ya Mungu. Mwangalie, saba. Loo, Yeye anahesabu kwenda mbele, akianzia na moja. Anaanza na wakati wa kwanza wa kanisa Lake. Hiyo ndiyo iliyokuwa mifano Yake duniani. Kuna nyakati saba za kanisa. Yeye aliumba ulimwengu katika siku saba; siku ya saba akapumzika. Hiyo ndiyo namba Yake ya mwisho katika uumbaji Wake. Alipumzika.

84 Angalia, Yeye huhesabu moja kwa moja kwenda mbele, si kinyumenyume. Anaenda mbele. Yeye huanzia kwenye wakati wa kwanza wa kanisa Lake, ambao ulianza 33 B.K., Naye akaanza kuhesabu kinyumenyume. Alihesabu nyakati Zake za kanisa. Huko kulikuwa ndio kuzaliwa kwa Kanisa, kwenye

Siku ya Pentekoste. Alininii. . .Anaanza kuhesabu. Anaanza kuhesabu nyakati za kanisa. "Wa kwanza, ulikuwa ni Efeso, namba moja; mbili, Smirna; tatu, Pergamo; nne, Thiatira; tano, Sardi; sita, Filadelfia; saba, Laodikia." Umechelewa zaidi kuliko unavyofikiria. Umechelewa zaidi kuliko unavyofikiria. Kuhesabu kumekwisha. Inayofuata ni "sifuri," twendeni. Kila kitu kiko tayari. Kuhesabu kumekwisha.

85 Wakati John Glenn, mwanaanga wetu, alipoingia katika ile tyubu kubwa, aruke, taifa lilisimama kimya kabisa. Hawakujua, ile asubuhi alipoondoka. Wakati alipoondoka, aliingia kwenye ile tyubu, na kila mtu alikuwa akilia, na kungojea, na kuangalia kile kitakachotukia. Taifa lilisimama limeduwaa. Mliona ninii. . .Televisheni zote zikitangaza, na kila kitu, ili kila mtu aweze kuona jambo hilo. Jicho la kawaida lisingeweza kuiona huko, kwa sababu waliliweka kwenye televisheni. Mnakumbuka jambo hilo.

86 Ndipo alipowekwa ndani ya tyubu hiyo vizuri sawasawa, na alipowekwa, walianza, "Kumi, tisa, nane, saba, sita, tano, nne, tatu, mbili, moja, sifuri," huyoo akaondoka. Ni jambo gani lilitukia? Wakati ule wenzo mkubwa ulipovutwa, zile atomi zilianza kushika moto, zikaanza kupasuka, moto ukaanza kuruka, moshi ukaanza kutokea, na ile tyubu kubwa mno ikaruka hewani, ikaingia kusikojulikana, huko ng'ambo mahali fulani. Aliruka katika mafanikio ya mwanadamu, yale makuu sana aliyowahi kupata. Lakini hebu niwaambie, hicho ni kitu kidogo sana.

87 Moja ya asubuhi hizi, mafanikio ya Mungu, ya wanaanga Wake waliopanda wakaingia katika Yesu Kristo, waliokwisha zaliwa mle na Roho Mtakatifu, wakajazwa na nguvu Zake! Moja ya asubuhii hizi, ulimwengu mzima utakuwa ukipiga makelele, na kuomboleza na kusaga meno, watakapoona kwamba wamelikosa. Wakati yule Tai mkubwa, akitiwa nguvu na Roho Mtakatifu na Moto, atakapoanza kutandaza mabawa Zake, wanaanga wataruka waingie angani, kwenda kumlaki Bwana Arusi; wakati Bibi-arusi atakapoondoka, katika nguvu za mwanaanga wa Mungu Mwenyezi Ambaye alimtuma Yesu Kristo duniani, katika umbo la Roho Mtakatifu, amelipitisha kanisa kwenye mafanikio haya!

88 Mpaka, sasa Yeye anapata Nguvu za kufufuka ndani yake, apate kuruka kupita mambo ya dunia, tukimwona ndani humu Kanisani, akijithibitisha Mwenyewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Naam, bwana. Kuhesabu kinyumenyume hata kumekwisha. Kila wakati wa kanisa umepita tayari. Tunaishia katika ule wa Laodikia.

89 Ingia ndani, ndugu yangu, dada. Pata nguvu. Nguvu hiyo haitakudhuru ukiingia ndani na kujazwa hiyo. Ingia katika Kristo, wala hutajali ulimwengu unasema nini. Hawezi

kukudhuru kamwe, hata hivyo. Wewe ni salama. Umeingizwa ndani.

90 Yesu Kristo ndiye tyubu yetu kuu, yenye utukufu ya Mwanaanga, ambayo tutakuwa ndani yake, ambayo itaendeshwa na Roho Mtakatifu na nguvu na Moto, wakati itakapoanza kuruka juu moja ya asubuhi hizi. Moto wa Roho Mtakatifu utashuka nchini namna hiyo, na, wakati watakaposhukiwa hivyo, Kanisa litainuliwa juu. Na mataifa yote yatasimama, hawatahitaji televisheni, watamwona. Kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri, wakati akienda zake huko juu, kuingia katika milki zenye utukufu za—za Mbinguni, apate kuolewa na Bwana arusi Wake. Mungu na atusaidie kuishi kwa ajili ya siku hiyo!

Na tuinamishe vichwa vyetu.

91 Je! umepanda kigari cha farasi leo, je! unaendesha baisikeli, unaninii. . .motokaa, ama je! umeingia mawinguni katika ndege? Kama umefanya hivyo, nina jambo la kukwambia. Kuna wakati wa mwanaanga unaoendelea sasa. Mbona usije na kuingia kwa Mwanaanga? Loo, ninajua linasikika ni la kutisha. Mtu wa kwanza aliyepata kuingia ndani ya ndege, aliogopa karibu azirai; wa kwanza aliyekuwa na motokaa, mnajua vile ilivyotukia; bali sasa ni kitu cha kawaida. Loo, ndugu, dada. Yesu Kristo yupo hapa, ile tyubu kuu ya Mwanaanga tunayopaswa kuingia ndani yake. Mawingu yakiwa yako juu yetu, hayatamaanisha chochote; Yeye atavunja kila wingu la shaka, kila kitu cha kutokuamini, na kuruka kwenda kuingia huko angani.

92 Kama hujaingia ndani Yake, bado, una nafasi alasiri ya leo. Je! ungeweza kuinua mikono yako, na kusema, "Niombee, Ndugu Branham, nipate kutembea niingie mahali pale ambapo ninaweza kuona kila Neno ambalo Mungu aliahidi, ninaweza kusikia na kuhisi ku—kudundadunda kwa Nguvu za Mungu ndani yangu, ili kwamba nipate kujua ya kwamba ninii yangu. . .ulimwengu huu na kadhalika vimenitoka"? Mungu akubariki. Angalieni tu mikono hiyo. Jamani, loo, jamani! Wote, kila mahali.

93 Baba yetu wa Mbinguni, Unaiona mikono yao. Mimi nina wajibu tu wa kulihubiri Neno. Wewe, hao ni Wako. Ninawakabidhi Kwako. Ni wako. Jalia Roho Mtakatifu sasa . . .

94 Na jalia waone jambo hilo, mafanikio haya. Wanayaona katika mambo ya kawaida; basi kama tukiangalia nyuma, tunayaona kiroho. Wewe upo hapa, Bwana. Uliahidi, kabla tu ya wakati wa mwisho haujaja, ya kwamba kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma na Gomora. Nasi tungeangalia nyuma na kuona siku hizo, tuangalie kule na kuona ambapo wahudumu wawili, maarufu, wa kimalaika, watu waliotiwa mafuta, walishuka wakaenda Sodoma na kuhubiri katika zile siku za Ibrahimu,

wakimwita Lutu atoke. Halafu kulikuwa na mmoja ambaye alikaa na Ibrahmu, na huyo alikuwa Ndiye Yule aliyekuwa amefanya ile ishara kwa Ibrahimu. Hao wengine, huko Sodoma, walifanya ishara yao.

95 Na, Baba, mambo mengi sana yangeweza kusemwa papa hapa, labda kanisa lisingefahamu. Bali ninaomba ya kwamba Wewe utawapa shauku kubwa sana ya Hiyo, Bwana, hata watakuja na kuona ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho, wakati wa mwanaanga. Ninaomba, Baba, ya kwamba watatambua si kujaribu kukanusha waliyokuwa nayo, ni kujaribu tu kuwapa ya zaidi, neema ya kunyakuliwa, kwa maana saa itakuja ambapo itatubidi kuwa na Nguvu za unyakuo; si kuponya mwili tu, bali kuubadilisha katika dakika moja, katika kufumba na kufumbua jicho. Kristo atakuwa ni halisi sana ndani ya miili yao mpaka anaweza kuubadilisha mwili, kwa mauti Yake kuu na yale aliyonunua. Jalia wachukue hili, leo, ile Ishara niliyonena habari zake jana usiku, waishike mbele zao na waingie katika wakati huu wa Mwanaanga (tujalie jambo hilo, Baba), ambako maono, nguvu, na ulimwengu wa ng'ambo ya pili, unaojulikana, na, Ee Mungu, ambako siri zote kuu za Mungu zinafunuliwa katika Mihuri hiyo Saba na kujulikana kwa wanadamu. Tujalie, Baba.

96 Hao ni Wako sasa. Ninatambua ya kwamba miito ya madhabahuni ndiyo tunayofanya, lakini, Bwana, Wewe ulisema, "Wote walioamini." Ninaomba ya kwamba utawapa imani, ya kuamini. Wako mikononi Mwako, Bwana. Na kama kamwe sitaona, wala wao wasinione tena, mpaka tutakapokutana kando Yako, tutajua wakati huo kama tunavyojulikana. Ninaomba ya kwamba utawasaidia. Na jalia sote tuwe Kule, salama, tumebebwa na neema ya ajabu sana ya imani yetu kuu ya mwanaanga tuliyo nayo katika Yesu Kristo, ambako tuko katika nyumba moja pamoja na Yeye. Amina.

97 Sasa, hebu dakika moja tu, tutawaombea wagonjwa. Mungu, tuliahidi kufanya hivyo. Tunataka kufanya hivyo. Na sasa ninataka kusema hivi, ya kwamba katika juma zima lote hili . . . sasa tuko na kama dakika kumi na tano, ishirini sasa. Nimekata machache, kwa hiyo nina kama dakika kumi na tano, ishirini bado, mpaka tunapoweza kufanya jambo hili.

98 Sasa, jambo la kwanza ni kwamba, mambo haya tunayozungumza habari zake, je! ndivyo yalivyo, ama sivyo? Tunajua Biblia ililiahidi, bali je! Yeye yupo hapa? Mungu yupo hapa kufanya yale sisi . . . yale Yeye aliyoahidi kwamba atafanya. Mungu yupo hapa. Unaona, tumepita kwenye kunena kwa lugha. Hilo—hilo ni sawa, unaona. Tumevuka mambo haya madogomadogo. Na, unaona, tumefikia mahali sasa ambapo hatuna budi kuwa na imani ya mwanaanga, yaani nguvu za mwanaanga kutambua ya kwamba sisi tuko katika Kristo tayari,

kumpata tu Kristo zaidi, unaona, kutuinua juu tuingine katika ulimwengu wa Roho.

99 Ule mtindo wa kale wa kuomba, kuweka mikono juu ya wagonjwa, hilo ni jambo zuri. Hizo zilikuwa ni siku za Luther, ewe rafiki, huko nyuma kwenye motokaa, ama kadhalika. Tumepita hayo sasa.

100 Kumbuka, Yesu alikuja kwa Wayahudi, siku za kale, Yairo alisema, Yairo alisema, "Njoo uweke mikono Yako juu ya binti yangu, naye ataishi." Lakini yule Mrumi alisema, "Mimi sistahili Wewe uje, sema tu Neno." Unaona? Kutambu-. . . Alitambua nguvu za Kristo, ya kwamba Yeye alikuwa juu ya mambo yote.

101 Sasa, kama Kristo yuko juu ya mambo yote, Yeye—Yeye hana budi kutimiza Neno Lake. Yeye ni Mfalme. Yeye ni Mungu. Hana budi kutimiza Neno Lake, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya." Sasa, kwa habari za kumponya mtu fulani, hakuna mtu anayeweza kufanya hivyo, kwa kuwa limekwisha kufanyika tayari. Limefanywa tayari. Ni suala la kulitambua tu jambo hilo, unaona, kutambua ya kwamba Yeye yuko miongoni mwetu. Je! mnaamini hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa ombeni kwa dakika chache, mseme, "Mungu, turehemu."

102 Baba wa Mbinguni, ili kwamba watu wapate kujua; huenda kukawa na wageni hapa, ili kwamba wajue ya kwamba haya ninayonena habari zake ni kweli. Mi—mimi niko katika njia yangu dhaifu na nyenyekevu, Bwana, ninajaribu kuileta Injili vizuri nijuavyo. Bwana, jalia watu wasiangalie sarufi zangu na watambue tu yale ninayojaribu kusema. Ninaomba ya kwamba utathibitisha hili na kulifanya halisi, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu. Amina.

103 Sasa, enyi marafiki, labda kuna kadi mia mbili ama mia tatu za maombi hapa. Ingekuwa ni vigumu kwangu kuzichukua hapa, mojamoja. Ama, baada ya kuwachukua wanne ama watano hivi wa huo utambuzi, ningekuwa nimelala sakafuni, labda, huenda ikawa, ama mdhaifu sana hata nisingejua. Ono, unapoona ono, halina budi kufasiriwa, pia, mwajua. Mara nyingi si hivyo tu hasa, inapaswa kuninii tu . . .

104 Sasa wewe unafanya hivyo, wewe mwenyewe, imani yako mwenyewe ndiyo inahusika. Imani ya yule mwanamke ilimgusa Bwana Yesu, naye aliamini ya kwamba Yeye alikuwa—alikuwa ni Mwana wa Mungu. Nayo ikavuta nguvu kutoka Kwake, zikamwingia yeye, ikampa haja yake, Naye akageuka na kumwambia ugonjwa wake ulikuwa umeponywa.

105 Unaona, "Imani yako *imekuokoa*." Sasa kuna wasomi wanaoketi hapa, ninajua. Neno hilo ni "sozo." "Neno lako *limekuokoa*." "Imani yako *imekuokoa*." Kama tu vile imani yako inavyokuokoa na dhambi, imani yako inakuokoa kimwili, unaona, kutokana na maradhi. Sasa huna budi kuliamini.

106 Sasa ninawaomba wote mwe kimya na mwe na kicho sana, kwa dakika chache. Na jalia Roho Mtakatifu sasa, angalau tu watu wawili ama watatu tu kwenye kusanyiko hili ndio tu ninaomba, mpate kuona kwamba si kitu kinachojiendesha chenyewe tu na kadhalika. Roho Mtakatifu yupo hapa kujidhihirisha Mwenyewe.

107 Sasa mtu fulani miongoni mwa wasikilizaji. Sasa, simjui hata mtu mmoja, nje ya Dada yangu mpenzi Upshaw anayeketi hapa, ninayeweza kumwona katika wasikilizaji wakati huu, ambaye ninamjua. Ni yeye peke yake. Na sasa siwezi . . .

108 Ni kama tu dhamiri yako. Unaona, dhamiri yako ya ndani ndiko unakootea ndoto.

109 Nilifanyiwa uchunguzi wa mwili, miaka kadhaa hapa, miaka mitatu iliyopita, kwa mawimbi ya wakati, mawimbi ya ubongo, mwajua. Nao madaktari wakaja wakasema, "Aisee, wewe ni mtu wa kuchekesha."

Nikasema, "Kuna nini?"

110 Akasema, "Unajua nini?" Kasema, "Ungeweza kuota ndoto ukiwa uko macho kabisa."

Nikasema, "Ati nini?"

Akasema, "Unaweza kuota ndoto wakati ukiwa macho kabisa." Nikasema . . .

111 Akasema, "Hii *hapa* dhamiri yako ya kwanza," kasema, "inaongozwa na ninii zako saba, ama hisi zako sita; kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kunusa. Dhamiri yako ya kwanza inafanya kazi tu mradi wewe uko katika hizo hisi sita." Kasema, "Hii *hapa* dhamiri yako ya ndani." Kasema, "Wakati hizi ziko kimya, basi unaingia katika dhamira yako ya ndani. Wakati hizi zimekaa kimya, wewe umelala, na unaenda na kuota ndoto, sehemu fulani yako inaenda kule. Ndipo wakati unaporudi *huku*," kasema, "ndipo unakumbuka uliyoota wakati ulipokuwa hutumii hisi zako za kugusa, kuonja, kuona, kunusa, na kusikia." Unaona? Kisha akasema, "Huyo ni mtu wa kawaida."

112 Kasema, "Hatujawahi kuona jambo hilo. Lakini zako zote mbili zimekaa papa hapa pamoja," kasema, "mawimbi yako yote mawili ya wakati, kutoka dhamiri ya ndani na dhamira hiyo nyingine yako. Wao hawajawahi kusikia kitu kama hicho kabla, maishani mwangu." Akasema, "Ajabu, ungeweza kuota ndoto, umesimama na ukiwa macho kabisa."

Nikasema, "Daktari, ulipata kusikia habari kuhusu ono?"

Akasema, "La, sidhani nimepata kusikia."

Nikasema, "Je! wewe ni mwamini?"

113 Akasema, "Mimi ni Mpresbiteri, Ndugu Branham, lakini," akasema, "hivyo tu." Akasema, "Mchungaji anakuwa na watu kule, kila Alhamisi usiku," kasema, "yote ninayosikia

ni 'Mpresbiteri, Mpresbiteri, Mpresbiteri.'" Kasema, "Hata siendi kule."

Nikasema, "Je! ulipata kusoma katika Biblia?"

Akasema, "Nimeisoma."

114 "Je! ulipata kusikia yale wale manabii wa kale, wa Agano la Kale, walivyoingia katika kiwango kingine na mambo kama hayo."

Akasema, "Hayo ndiyo unayozungumzia?"

Nikasema, "Ndiyo." Na nikasema . . .

115 Akasema, "Vema, hilo lingekuwa ni jambo la ajabu sana. Aisee, Ndugu Branham, unapaswa kwenda . . . "

116 Nikasema, "Tayari nimekwisha kuhojiwa na akina Mayo, unaona." Nami nikasema yeye . . . Nikasema, "Lakini, angalia, hivi wewe kamwe huota ndoto, daktari?"

Akasema, "Loo, hakika."

117 Nikasema, "Niotee ndoto, basi. Hebu lala usingizi tu na uniotee ndoto, uniambie la kufanya. Usingeweza kufanya hivyo. Lakini yeyote yule anayekuongoza, angeweza kukupa ndoto, juu yangu, halafu ungeweza kuamka na kuisimulia."

118 Wala mimi siwezi kufanya hivyo, pia. Siwezi kusema kuna nini, *hapa* ndani. Haina budi kuwa ni Yeye anayefanya jambo hilo. Na imani yako, katika Yeye, inathibitisha Neno hili. Ninii tu, mwanamke yule, haidhuru mtu yeyote alisema nini, aliamini kama angeweza kugusa vazi Lake, ingekuwa, ingetukia. Sasa, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa hivyo tu ndivyo ilivyo.

119 Unaona, wakati unapoona uigaji, na kadhalika, rafiki yangu, kwa namna fulani kidogo linakuvuruga. Lakini endelea tu, hata hivyo. Itakuwa—itakuwa ni sawa, unaona. Sasa, angalia, huna budi kuzaliwa kwa kusudi la jambo hilo. Unazaliwa, na karama zote za kawaida zinakuja kwako. "Karama na miito hata havina majuto." Kama vile mwanadamu . . . Kama vile nilivyokuwa nikizungumza na Paul Cain, muda mfupi uliopita, juu ya . . . Kama vile Ernie Ford, na Red Foley, na Elvis Presley, hao jamaa walio na hivyo vipaji vikubwa vya kuimba, na kuvitumia kwa ajili ya ulimwengu. Mungu aliwapa hivyo vipaji, na angalia kile wanachofanya na hilo.

120 Ni kama vile Yuda Iskariote akipata vipande thelathini vya fedha kutokana na hicho, kwa Yule aliyemtunukia hilo. Wanapaswa kuwa wakivitumia kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Na wakati unapochanganya mambo hayo, nafikiri hawapaswi kuruhusiwa kuimba wimbo wa dini; hiyo ni kazi ya kanisa na watu wake, si kuvitumia huko nje kufanya unafiki zaidi. Niliingia Afrika Kusini, nao walikuwa ninii sana, "Mbona, Elvis Presley ni mvulana wa kidini sana, yeye anaimba nyimbo za dini." Loo! Hilo halimaanishi kitu. Kwangu mimi, ni Yuda

mwingine. Na hao watu wote wanaochukua vipawa hivyo vya Mungu na kuvipotosha.

121 Hata kwa mhudumu ambaye atavichukua na kuvipotosha kwa kanuni ya imani, badala ya Neno la Mungu, na kutumia ushawishi wake kushawishi kwa kanuni ya imani wala si kwa Neno la Mungu, ni Yuda wa pili. Mimi sininii . . .

122 Haikunipasa kusema jambo hilo. Ninyi, kama nimewaudhi, samahani. Si—sipaswi kusema mambo hayo hapa. Vema.

Hili hapa jambo moja, ninaweza kusema anayoniambia. Ninyi ombeni.

123 Sasa, Bwana, Neno moja kutoka Kwako litamaanisha zaidi ya ningeweza kusema maishani mwangu mwote. Ninaamini. Uliahidi jambo hilo. Mimi ni Wako. Jalia waone ya kwamba Roho Wako yupo hapa, ndipo wakati watakapokuja kwenye mstari huu wa maombi, kuombewa, watafahamu, Bwana. "Maombi ya imani yatawaponya wagonjwa." Ninaomba ya kwamba wataona ya kwamba si mtumishi Wako. Ni Wewe. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

124 Ketini tu kimya, muda kidogo. Siwezi kufahamu hili. Mnasema, "Ndugu Branham, ati nini?" Siwezi kuwaambia. Ninaweza tu jinsi anavyonionyesha.

125 Yesu alisema, "Sitendi neno mpaka Baba anionyeshe, kwanza. Ninalomwona Baba akifanya, ndivyo anavyofanya Mwana vile vile."

126 Hapa, kama mmeinua vichwa vyenu, angalieni hapa. Mnaona, akiketi papa hapa mwishoni mwa safu, maskini yule bibi? Ana ugonjwa wa akina mama, ugonjwa wa akina mama. Hiyo ni kweli, ewe msichana. Hiyo ni kweli, njia ya kutoa uchafu na kila kitu. Hiyo ni kweli, utainua mkono wako? Sikufahamu kabisa. Ni msichana mdogo, ipo Nuru papo hapo juu ya dada, papo hapo mwishoni mwa safu pale. Ni msichana mdogo, kijana mwanamke mwenye nywele . . . Ninamwona bafuni. Kama utaamini sasa hivi! Sasa, unajua ya kwamba jambo fulani lilitukia wakati uo huo. Mara moja tu, Kitu fulani kilipitia moja kwa moja ndani yako. Sivyo? Hicho kilikuwa ni uponyaji wako. Unaona, hapo ndipo wakati ulipopata nafuu na ugonjwa ukaondoka. Imani yako ilikuokoa.

127 Hivi hilo silo jambo lile lile Bwana wetu alilofanya? Yako . . . Alikuwa anatokwa na damu, mwanamke yule. Aligusa vazi Lake, naye akageuka. Alihisi hilo. Akaangalia. Akasema, "Ni kutokwa kwako na damu," akasikia kumekoma. Hilo ni jambo lile lile Yesu Kristo alilofanya. Ni kitu gani? Ni Yeye. Loo, na—najua mmeona kila kitu, bali mimi-mimi ninawajibika tu na jambo hili. Mungu anawajibika tu kwa Neno Lake.

128 Hapa, kusudi mpate kujua. Anayeketi papo hapo nyuma yake ni bibi mmoja ameketi pale akiwa na kifafa, anaanguka

kifafa mara kwa mara. Kama unaamini, Mungu atakuondolea hicho kifafa, mama. Atafanya hivyo kama utaamini. Amini. Usitilie shaka.

129 Mnaona ninalomaanisha? Sasa mtu fulani kwenye sehemu *hii* hapa, mahali fulani papa hapa ndani, ili mpate kuona. Mnaona, jambo ni kwamba, mnaangalia . . .

130 Hebu niseme jambo hili moja kabla sijaondoka sasa, kusudi nipate kujipumzisha.

131 Unaona, hilo, hilo mtu linakufanya. Hilo linachukua nguvu nyingi zaidi kuliko zile nilizohubiria. Hakika. Unaona, huyo ni wewe ukitumia karama ya Mungu. Kama Mungu alikuwa ametoa karama mo- . . . ama kutoa o—ono moja kwa moja . . . Kama vile Yesu alivyomwona Lazaro akifa, na akaondoka nyumbani na kungojea; kisha akawaambia yale yangetukia, na kisha akarudi na kufanya jambo hilo, Yeye hakusema kamwe alikuwa mdhaifu. Lakini maskini huyo mwanamke mmoja, huyo alikuwa ni yule mwanamke akitumia karama ya Mungu. Ni wewe. Karama ya Mungu, wakati Yeye anapoitumia haikuchoshi. Lakini wakati wewe unapoitumia; ndipo Mungu amekuweka mikononi Mwake, na kusema, "Hili litakuwa *hivi*, hapa na hapa na hapa. Jambo hili litakuwa hivi." Hivyo ndivyo ilivyo; halikusumbui. Lakini wakati hao watu wanapoingia na kuvuta hiyo, hilo ndilo linalokuchosha. Hilo ndilo linalokuchosha.

132 Watu siku hizi, Wakati wa Kanisa la Laodikia, kule kuhesabu kinyumenyume kwa mwisho. Je! mliona, hivi majuzi usiku, kabla tu ya papa wa Roma kufanya ziara yake ya kwanza, katika historia yote, ya kwenda Yerusalemu? Kamwe hapajawahi kuwa na papa huko Yerusalemu, aliyetumwa, hapo nyuma. Mnaona, alitoka Rumi akaenda Yerusalemu. Kanisa, mwezi unawakilisha kanisa, ukiakisi nuru ya jua, jua lisipokuwapo. Mungu hufanya ishara mbinguni kabla Yeye hajalitangaza duniani. Je! uliona kwamba mwezi uliingia giza kabisa? Yerusalemu ndilo kanisa la zamani sana ulimwenguni. Mnaona? Na wakati Baraza hili la Ekumeni na vitu hivi ambavyo . . .

133 Wewe mtu, natumaini, kama uko hapa, ya kwamba jambo hili unalipata vilivyo. Unapojiunganisha, hivi hujui unachukua alama ya mnyama, rafiki yangu? "Loo," unasema, "Kama nikiliona likitukia!" Umeisha chelewa sana wakati huo. Tayari umefanya jambo hilo. Unaona? Umechelewa sana wakati huo. Kumbuka, walikuja kununua Mafuta, bali hakukuwako . . . wasingeweza kufanya jambo hilo.

134 Je! uliona jambo lililotukia, kile kilichoufanya mwezi kuingia giza? Ulimwengu uliingia katika njia yake. Vivyo hivyo ulimwengu uliingia katika Nuru ya Maandiko, miongoni mwa Wapresbiteri, Wamethodisti, Wabaptisti, Wapentekoste, na sisi sote. Hiyo ndiyo sababu ya kuingia giza.

135 Na hivi uliona Wakati wa Kanisa la Laodikia, pia, ulikuwa ndio wakati pekee wa kanisa ambao Yesu alikuwa yuko nje, akijaribu kuingia ndani? Hivi uliona ya kwamba kamwe hakusema "achana nao"? Yesu ni Neno (hiyo ni kweli), Neno lililodhihirishwa. Sasa Yeye. . .Sasa sikilizeni. Yeye hakuwa, unaona, ameondoka na kuwaacha, bali Yeye alikuwa akijaribu kupata ushirikiano mahali fulani. "Yeye atakayefungua mlango, nitaingia pamoja naye, nile pamoja naye, naye pamoja nami." Lakini, hakuna mlango, unaona; akijaribu tu kuingia, yuko nje. Hawamkatai mwanadamu, wanamkataa Mungu.

136 Je! unaamini jambo hilo, maskini msichana unayeketi pale ukiwa umevaa miwani? Naam. Unaamini jambo hilo? Ulikuwa na mawazo ya kina papo hapo. Macho yako yataponywa kama utaamini.

137 Sasa hebu niwaambie. Mtu fulani anasema, "Amevaa miwani, ndiyo sababu alijua jambo hilo." Hapana.

138 Angalia hapa. Njoo hapa; si kuja hapa, hebu niangalie tu kwa dakika moja tu. Je! unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama mtumishi Wake? Je! unaamini hilo? Unaamini. Ulipaswa kuamini, ukiwa na mawazo hayo uliyokuwa nayo wakati huo, ukiwazia jinsi ilivyokuwa ni la ajabu, "Huo ulikuwa ni ufunuo mkubwa jinsi gani, wa mwezi, na kuwakilisha hilo." Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli, inua mkono wako.

139 Sasa ningewezaje kujua yale huyo mama aliyokuwa hata akiwaza moyoni mwake? "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, huyatambua mawazo yaliyo ndani ya moyo."

140 Sasa mwombee mtu fulani, ama fanya jambo fulani. Haya, haya ndiyo yanayojitokeza moyoni mwako sasa hivi. Haya, haya ndiyo yaliyo moyoni mwako. Una ndugu wawili ambao unawaombea, nao wote wametawaliwa na pombe. Kama hiyo ni kweli, inua mikono yako. Vema.

141 Vema, mnaona, haya basi. Mnaona? Mnaona hapo? Mnaona? "Ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Hivi hamwoni jambo hilo, enyi marafiki? Tumepita kwenye kunena kwa lugha. Tuko wakati wa mwanaanga.

142 Hapa, huyu hapa mtu papa hapa mbele ya huyo mama, ameinamisha kichwa chake. Ana nywele chache, amevaa koti jeupe, amevaa miwani. Ana shida ya kiroho ambayo yeye ananinii. . .John Thom-. . .

143 Loo, ngoja kidogo, ninamjua mtu huyo. Ngoja kidogo. Samahani. Ni—ninamjua mtu huyo. Hiyo ni kweli. Ninaamini ni—nilikutana naye wakati mmoja, mahali fulani. Siwezi kukumbuka ni wapi. Ninaamini ilikuwa ni kule Tucson, hapa si muda mrefu uliopita, niliwapa mikono kwenye. . .Na—na hiyo ni kweli.

144 Lakini ulikuwa ukimwita Mungu papo hapo. Una shida kubwa ya kiroho ambayo hujui jinsi ya kuithibiti. Angalia, Bw. Thomas, usiwe na wasiwasi, itakuwa sawa. Sasa ili kwamba upate kujua ya kwamba hii . . . Ulisema, "Vema, a—alimjua mtu huyo." Vema, huyo anayeketi karibu naye ni mke wake. Sikujua hiyo ilikuwa ndiyo shida ya Bw. Thomas. Yeye, atashuhudia hilo. Lakini mke wake anayeketi karibu (naye) na yeye pale, ana shida ya sikio ambalo linamuuma. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli. Vema.

145 Hapa, mchukue mama huyo mwingine, bibi huyo anayemfuata. Angalia huku, mama. Je! unaniamini mimi kwamba ni mtumishi Wake? Masikini bibi huyo aliyevaa koti jekundu, je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Una shida fulani, pia. Unaumwa na kichwa wakati wote. Je! unaamini Mungu atakuponya maumivu hayo ya kichwa? Kama unaamini, inua kichwa chako, mikono, na useme, "Ninaamini jambo hilo." Vema. Hilo ni sawa. Unaona? Vema, kama unaliamini jambo hilo!

146 Hapa, masikini mama huyu anayevaa koti la bluu, anayeketi karibu naye. Je! unaamini, dada? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa moyo na kukufanya mzima? Unaamini? Vema, unaweza kupokea hilo.

147 Mama anayeketi karibu naye, bibi mzee, mwenye mvi. Je! unaamini Mungu anaweza kukuponya, pia, shinikizo la juu la damu, na kukufanya mzima? Vema, unaweza kupokea uponyaji wako. Unaona?

148 Mama anayeketi karibu naye, una shida ya masikio yako, pia. Je! unaamini Mungu huponya shida ya sikio? Basi unaweza kupokea uponyaji wako.

149 Mama anayeketi karibu naye. Je! unaamini, mama, kwa moyo wako wote, ya kwamba Mungu huponya? Una kitu fulani unachoombea. Je! unaamini kwa moyo wako wote ya kwamba Mungu huponya? Vema, kama unaamini hivyo kwa moyo wako wote, shida yako ya tumbo inaweza kuponywa. Unaweza kwenda nyumbani, ule chakula chako cha jioni na uwe mzima.

150 Bwana, wewe unayeketi karibu na—naye. Je! unaamini ya kwamba—ya kwamba Mungu anaweza kukuponya, pia, na kukufanya mzima? Ungekubali jambo hilo?

Ni wangapi, ninyi wengine mliosalia, mtaamini kwa moyo wenu wote? Hakika, mtaamini. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

151 Shida ya tumbo, ugonjwa wa moyo, Mungu huyaponya yote, anayaponya. Hiyo ni kweli. Kama mtaninii . . .

152 Mtu anayeketi karibu naye, anaumwa na mgongo. Je! unaamini Mungu huponya shida ya mgongo, bwana? Unaamini?

153 Mama anayeketi karibu nawe ana shida ya mgongo, pia. Je! unaamini Mungu huponya shida ya mgongo, mama? Vema, unaweza kupata wako. Hiyo ni kweli. Loo, jambo pekee unalopaswa kufanya . . .

154 Bibi anayeketi karibu na huyo ana shida ya utumbo mpana. Hiyo ni kweli. Je! unaamini ya kwamba Mungu ataponya shida yako ya utumbo mpana, bibi? Unaamini?

155 Hapa, moja kwa moja tukishuka katika mstari, angalia. Kuna jeraha la akili limekaa pale. Unaamini Mungu anaponya jereha la akili? Unaamini? Unaweza kuponywa.

156 Huyo anayeketi karibu na wewe ana kifafa. Unaamini Mungu huponya kifafa?

157 Mtu anayeketi karibu na wewe ana . . . ana shida ya macho. Je! unaamini Mungu huponya shida ya macho, bwana?

158 Huyo anayeketi karibu na huyo, mvulana huyo mdogo, yeye pia ana kifafa. Je! unaamini Mungu huponya kifafa?

159 Mpenzi wake anayeketi hapo pamoja naye ana shida na kichwa chake. Je! unaamni ya kwamba Mungu ataponya shida yako ya kichwa, mama? Vema, unaweza kuupokea.

160 Amina! Ni kitu gani? Neno la Mungu kwa ajili ya siku hii ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Yesu Kristo katika nguvu za mwanaanga! Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

161 Kadi zetu za kwanza za maombi zilikuwa ni zipi? [Mtu fulani anasema, "ni za A."—Mh.] Za A. Watu wote walio na kadi ya maombi A, simameni upande huu. Sasa njoni haraka, kadi ya maombi A, wakati upako unapofanya kazi jinsi unavyofanya. Kadi ya maombi . . . [Sehemu tupu kwenye kanda]

162 Papa hapa chini, ili kwamba niweze kushuka na kuwaombea hapa chini. Ninaamini ingekuwa ni bora zaidi. Njoni . . . [Mtu fulani anasema, "Je! unataka maiki? Unataka maiki ya shingoni?"—Mh.]

163 Shukeni mwende *hivi*, marafiki, huku chini upande huu ili tuweze kupanga mstari. Kadi zote za maombi A, wasimame kwanza, wamekuwa wakishikilia kadi zao kwa muda mrefu zaidi. Hebu kila mtu aliye na kadi ya maombi A, asimame upande huu hapa. Billy, shuka uende uone kama wako kwenye mstari.

164 Sasa kadi ya maombi B, hebu na wawafuate. Wote walio na kadi ya maombi B, wafuateni wale wa za-A. Nendeni, zungukeni kwenye marefu hayo mengine ya kanisa pale, mkiweza, na mpange mstari wenu uzunguke upande ule; A, B.

165 Kama tu mtaamini! Mwanaanga tu mara moja, tokeni kwenye motokaa na ndege. Hebu twendeni na tukaingie mpaka mambo yote yawe yanawezekana.

166 A, B, sasa mtu yeyote aliye na kadi ya maombi C, jiungeni moja kwa moja nao nyuma yao. Kadi ya maombi C, rudini hapa nyuma, mpitie *hapa*, marefu ya katikati ya kanisa, kisha mwende upande wa pili na mfanye mstari wenu pale. Kadi ya maombi A, B, C. [Mtu fulani anasema, "Huenda wengine wameondoka. Huenda kukawa na wengine zaidi. Ita tu kadi zote."—Mh.]

167 Nyuma *huku* sasa. Hiyo ni kweli, fanyeni mstari wenu papo hapo namna *hiyo*, namna hiyo. Geukeni vivi *hivi*, ili kwamba tuweze kuwa na uhakika kuingia mstarini. Kadi ya maombi A, B, C, hebu na wafanye mstari kwanza.

168 Shikilia tu kadi yako mkononi mwako, nitawaagiza baadhi ya mabawabu wachukue kadi zenu. Sijui jinsi tutakavyoweza kuwafanya wapange mstari kulingana na namba. Nafikiri itakuwa ni sawa, hata hivyo. [Mtu fulani anasema, "Ni sawa, Ndugu Branham."—Mh.] Waacheni tu.

169 A, B, C, sasa D. A, B, C, D, kadi ya maombi D. A, B, C, D. Je! kuna D zozote? Nafikiri nimemaliza. Kadi ya maombi A, B, C, D. Vema. Mtu yeyote aliye na kadi za maombi sasa, afanye mstari. Kila mtu aliye na kadi za maombi, ingieni kwenye upande wenu na mfanye mstari. Hakuna njia kwetu, hata kidogo, kuweza hata kufanya, kuwapanga kwenye mstari kikamilifu kwa namba.

170 Sasa ninataka kujua ni wangapi hapa ndani watakuwa wakiomba pamoja na mimi wakati mnaponinii...wakati tukiwaombea hawa wagonjwa. Sikilizeni, je! mnaninii...

171 Sasa, angalia, kama utapitia upande huu ili uombewe, useme tu, "Vema, nitaenda pale nione jinsi jambo hilo linavyotukia," ni afadhali ukae kitini pako. Haitatendeka. Unaona?

172 Sasa Yeye hawezi kufanya jambo lingine zaidi, wala hatafanya ishara moja zaidi mbele za watu. Hiyo ni kulingana na Biblia. Ninataka mtu fulani aniambie ishara moja zaidi aliyoahidi kufanya mbali na ile amefanya papa hapa. "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," na Malaki 4, na hizo ahadi ambazo alifanya, zote zinaishia kwenye jambo lile lile. Hakutakuwa na ishara nyingine itakayotolewa kwa kanisa. Jambo linalofuata utakaloona litakuwa ni kuruka kwenda Mbinguni. Watanyakuliwa.

173 Usininii, usikose jambo hilo, rafiki. Kumbuka, sikiliza Sauti yangu. Itakufuatilia maishani mwako mwote, kama hujaingia. Huko ng'ambo ya pili, wakati utakapokuwa ukiteseka kwa adhabu yako, na mahali ambako kulia na kuomboleza na kusaga meno, Sauti hiyo itapiga makelele huku na huko, utaisikia daima katika mahali hapo pa kuzimu panapochosha, penye mizuka. Usikose. Sasa ndio nafasi yako.

174 Sasa, loo, wako wengi sana tu! Sijui kama ningeweza kupata...Je! ingekuwa ni sawa, ninyi ndugu kuomba pamoja na mimi, kunisaidia kuwaombea? [Ndugu mmoja anasema,

"Naam."—Mh.] Sasa, hawa ni wahudumu, hapa? ["Naam."] Ni—nisingeondoka mahali hapa . . .

175 Sasa, angalia, nimesema mambo makali sana kuhusu ndege, motokaa. Kumbukeni, hizo ni nguvu farasi, pia. Zote ni nguvu-farasi. Kanisa linapaa juu tu, nguvu za Roho Mtakatifu. Tunahesabiwa haki kwa Roho Mtakatifu. Ninyi wahudumu mnajua jambo hilo, sivyo? Roho Mtakatifu hututakasa. Roho Mtakatifu hutujaza. Roho Mtakatifu hutupa nguvu za kunyakuliwa, unaona, tunapoenda juu.

176 Sasa, nisingeweza kuondoka nchini humu, na ninyi nyote mkifikiria ya kwamba nanii wenu . . . ya kwamba, "Loo, Ndugu Branham ni kitu fulani!" Hata. Hata sistahili kuketi pamoja na hao wachungaji. Si—sina kisomo. Mimi, ni mtu wa kipekee. Na hiyo ndiyo sababu Mungu ananiruhusu tu kufanya jambo hili dogo hapa, kuhakikisha tu yale mchungaji wenu amekuwa akiwafundisha. Wao ni watu wa Mungu.

177 Sikilizeni, kama wewe u mgonjwa, hupaswi kumgojea Ndugu Oral roberts, ama Ndugu Paul Cain, ama mimi, ama mtu yeyote. Mchungaji wenu mcha Mungu, mikono yake mitakatifu iliyotakaswa ikiwekwa juu yako, unajua ulimwita akuombee. Anaweka mikono yake juu yako wakati unawaka moto kwa homa; muda si muda unajua, katika siku chache huna hiyo homa, na umepona. Ni kitu gani? Ni imani ya mchungaji wako, pamoja na yako. Naam, bwana. Yeye si mtu baki. Yeye ni mtumishi wa Mungu, papo hapo kwenye mstari wa mbele, akiwa na Upanga ukatao kuwili mkononi mwake. Hakika. Hakika ndivyo alivyo.

178 Nitawaomba hawa wachungaji waje hapa, wasimame pamoja na mimi tunapoomba. Je! mtafanya jambo hilo, ninyi nyote? Njoni papa hapa na mninii tu . . . Nitashuka moja kwa moja niwe pamoja na ninyi, na hebu na tufanye mistari miwili papa *hapa*. Sasa wakati watu wanapoponywa, hawawezi kusema, "Unaona . . . " Ninataka mikono yako, mchungaji; ninyi, ndugu zangu. Na sasa tunaninii . . . ninyi mnaninii . . . Kama mtaninii tu . . .

179 Kama mkija, mkisema, "Vema, nitajaribu. Nitaninii . . . " La, msifanye hivyo. Msininii, msipachukue mahali pa mtu mwingine. Mnaona? Njoni, mkijua ya kwamba mtapata mlichoomba.

180 Hebu angalieni tu hapa, ni kundi la wahudumu la jinsi gani! Loo, jamani! Nimekutana na karibu watu hawa wote. Ninawajua. Ninawajua, kwa kukutana nao kwenye viamshavinywa, na—na kadhalika. Ni wacha Mungu. Ni watumishi wa Mungu.

181 Sasa angalieni hapa. Kwenye ile siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu alijitenganisha Mwenyewe, na ndimi za Moto zilikaa juu ya kila mmoja wao. Ile Nguzo kuu ya Moto ilijigawa, na kila mmoja alipokea sehemu ya Roho Mtakatifu, juu yao, kama

ndimi za Moto. Vema, kama ukiweka ulimi mmoja wa Moto, na ndimi mbili za Moto, pamoja, unapata nguvu maradufu ya zile ulizokuwa nazo kwa mmoja. Kumbuka, je! hivi si ilikuwa ni Ezekieli, katika ono lake la vile vijiti viwili mkononi, mnaona?

182 Sasa angalia hapa, angalia hapa mlio nao, watu wa Mungu hawa wote! Mbali na hayo, ni wangapi katika wasikilizaji huko watakuwa wakiomba, inua mkono wako? Angalieni hapa! Sasa, ninyi watu mlioko kwenye mstari wa maombi, angalieni jambo hili. Angalieni hapa ni akina nani watakuwa wakiwaombea, mamia ya watu.

183 Sasa Roho Mtakatifu yupo hapa sasa hivi, Yesu Kristo, akijithibitisha Mwenyewe, Yeye yupo hapa. Hawezi kufanya zaidi ya hayo. Sasa ni wangapi kwenye mstari wa maombi wanaamini hayo, inueni mikono yenu? Sasa hebu sisi sote.

184 Sasa nitamwomba Ndugu Borders, ama mtu yeyote, kiongozi wa nyimbo. Kiongozi wa nyimbo ni nani? Una maiki hapo? Vema. Nitawaomba baadhi yao waje hapa na kuimba ule wimbo, *Amini Tu*. "Mambo yote yanawezekana, amini tu."

185 Halafu wanapoimba wimbo huu, ninamtaka kila mtu awe katika maombi. Msi—msininii, isipokuwa iwe jambo la ajabu sana litukie, hata msiangalie juu.

186 Sasa inawabidi mwe wanyofu. Ni kati ya mauti na uzima, kwa baadhi ya watu hawa. Wapo moja kwa moja hapo wakiwa na kansa, na uvimbe, na TB, na kila kitu, wanakufa. Vipi kama huyo angalikuwa ni mama yako? Ni wa mtu fulani, kumbuka. Sasa iweni na kicho kwelikweli. Na wakati wanakapitia hapa nasi tuweke mikono juu yao. . . Ninashuka nije papo hapo chini pamoja na watu hawa. Na wakati wao, sisi, tunapoweka mikono juu ya watu hao, ninyi ombeni ya kwamba wataponywa.

187 Na sasa ninyi mlio kwenye mstari wa maombi. Sasa hebu ngoja ninii, ninaweza tu kuwaambia. Sasa, kule nyuma, na wote wale watakaokuwa katika mstari wa maombi. Mtakapopitia hapa, fanyeni jambo hili sasa, kama mtaninii—kama mtaniamini mimi. Angalieni, mtakapopitia kwenye mstari huu, na wakati ninii. . . Mkipita kwenye huo mstarini, kumbukeni tu, ni kama mnatembea chini ya vivuli vya Msalaba. Mnafanya. . . Watu hawa wanafanya vile vile hasa Yesu alivyosema wafanye. "Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Ninashuka hapo chini, kama nilivyosema pale mwanzo, nikitandaza wavu wangu pamoja nao, tupate kufanya kila kitu tuwezacho kuwasaidieni ninyi watu. Je! mtaamini?

188 Sasa hebu na tuombe, kwanza, maana ilisema. . . Mwajua, Petro alikwenda na akaomba pembeni kwenye chumba ambapo Dorkasi alikuwa, amekufa, halafu akaenda pale na kuweka mikono yake juu yake. Baada ya kuomba, alisimama akaenda pale na kuweka mikono yake juu yake. Eliya alitembea huku na huko sakafuni, mpaka Roho akaja juu yake, ndipo akaenda

na kulaza mwili wake juu ya mtoto mchanga aliyekuwa amekufa. Mnakumbuka jambo hilo? Sasa tutaomba, na halafu tutawawekea mikono mnapopitia mstarini. Nanyi mje hapa na, mara tu mikono hiyo itakapowagusa, simameni na ukubali imani yako, na uondoke uende, ukimsifu Mungu. Kuwa mwanaanga sasa unapopitia hapa, ruka tu utoke kwenye kutokuamini kote.

189 Baba yetu wa Mbinguni, hili linafikia kilele chake na wakati ulio muhimu sana, jambo kubwa sana linaloweza kutukia, kwa wagonjwa, ni hivi sasa. Ambapo, umati hapa wa mamia ya watu utakuwa ukipitia kwenye mstari wa maombi ya wahudumu ambao umewaita kutoka kwenye mazingira mbalimbali ya maisha, nao wamekutolea maisha yao, kwa kuliheshimu Neno la Mungu na wito wao.

190 Hapa kwenye kasha hili kuna leso, zinazokwenda kwa wagonjwa na wanaoteseka. Bwana Yesu, jalia kila mmoja wao apone, tunapozituma katika Jina la Yesu Kristo.

191 Na wakati wagonjwa hawa wanapopitia kwenye mstari huu, jalia kila mmoja wao, Bwana, awe na imani sasa. Jalia wafanye uamuzi mawazoni mwao, na kusema, "Nimekuwa nikichezacheza. Sitacheza tena. Kama nitaamini, nitaamini sasa hivi. Nimeona Neno lililo hai la Mungu likidhihirishwa. Ninajua, katika chumba hiki, Yesu Kristo yuko mahali fulani. Hakika yule ambaye Yeye anajidhihirisha kupitia kwake hatatwambia uongo, kwa maana Wewe ulisema, 'Kama kuna mtu aliye wa kiroho, ama nabii, na asemalo linatimia, basi msikieni."

192 Bwana Mungu, jalia hilo liwe niani mwa watu, ya kwamba ninajaribu kuwaambia ya kwamba Wewe hujafa, ya kwamba Wewe unaishi papa hapa sasa hivi, na Wewe—upako Wako uko juu ya Kanisa Lako na watu Wako. Jalia waponywe wanapopitia hapa. Ninaomba ombi hili katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

193 Sasa hebu na tuwe katika maombi, wakati Ndugu Borders ama yeyote yule atakayeongoza kuimba. Endeleeni kuinamisha vichwa vyenu, nami ninashuka kuja hapo sasa kusimama kwenye mstari huu hapa na kuomba pamoja na watu hawa.

194 [Ndugu Branham na wahudumu sasa wanamwombea kila mtu aliye kwenye mstari wa maombi, wakati kusanyiko linaomba, na kuimba, "*Amini Tu*." Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

> Bwana, naamini
> Kwa kuwa mambo yote yanawezekana, Ee Bwana, naamini;
> Ee Bwana, naamini, (hebu na tuinue mikono yenu tunapouimba), Ee Bwana, naamini,
> Mambo yote yanawezekana, Ee Bwana, naamini.

195 Mwajua, siamini nilipata kupitia katika mstari wa maombi maishani mwangu, ambapo nilishuhudia imani zaidi kuliko

niliyoshuhudia katika mstari ule. Kweli ndio mstari wenye nguvu sana wa maombi ninaamini niliopata kuwa nao Marekani, maishani mwangu, kuona mstari ukipita namna hiyo. Nina hakika tu kama vile jina langu lilivyo William Branham, nami ninasimama hapa kwenye jukwaa hili, ninyi wachungaji mtasikia kuhusu watu wenu ambao wamepitia kwenye mstari. Kweli ilikuwa ni imani kubwa, miongoni mwa watu walio bora sana niliopata kujua maishani mwangu, kulingana na njia pekee nimeishuhudia, kwa upako wa Roho Mtakatifu. Kwa kweli ulikuwa ni wa ajabu sana. Asanteni, enyi watu.

196 Sasa wote wale mnaoamini mmeponywa, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hilo hapo, sikilizeni hayo! Mungu awabariki.

197 Mungu awe pamoja nanyi hata tutakapoonana tena. Bwana akipenda, nitakuwa hapa juu ulipo huu Tulare. Hilo ndilo jina lake? Tulare, Tulare hapa juu, juma hili lijalo.

198 Sasa hebu sote na tusimame kwa miguu yetu, kwa dakika moja, wakati tukiruhusiwa kufumukana katika utaratibu wa kawaida. Na halafu watasambaza leso za maombi hapa, na kadhalika. Mungu awabariki.

199 Na Mungu awabariki ninyi ndugu mnaohudumu. Hilo ndilo linalolifanya halisi sana, wakati ninyi ndugu, kulikuwa na Paul Cain na wachungaji hawa wote, na wote wakisimama hapa, msaada mkubwa katika imani.

200 Kwa kweli nimefurahia mkutano huu, mno. Ninauhesabu kuwa mmoja wa mikutano muhimu sana niliyopata kuwa nayo Marekani. Nimekuwa na mingine iliyokuwa ni mikubwa zaidi.

201 Mungu akubariki, dada. [Dada Upshaw anasema, "Nilitaka tu kukupa mikono. Loo, haleluya!" Seneta William D. Upshaw aliponywa papo hapo kwenye ibada ya utambuzi ya Ndugu Branham huko Los angeles tarehe 8 Februari, 1951, baada ya kuwa kiwete kwa muda wa miaka sitini na sita—Mh.]

202 Mungu akubarki, Dada Upshaw. Hakuna juma linalopita ambapo siwazii juu yako na—na Ndugu Bill. Nitakutana na ninyi kwenye ile pwani Kule, dada, ambako mambo yote ya kale yamepita. Tutakuwa Kule siku hiyo. Amina.

203 Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu tunapomwomba mchungaji hapa, mmoja aje aturuhusu kuondoka kwa maombi rasmi. Na tuinamishe vichwa vyetu. Ndugu, Bwana akubariki.

Kuhesabu Kinyumenyume SWA64-0209
(Countdown)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 9 Februari, 1964, katika Uwanja wa Maonyesho wa Wilaya ya Kern, huko Bakersfield, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2008 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org